

Uhuru na Amani

GAZETI LA KANISA LA KIINJILI LA KILUTHERI TANZANIA TOLEO LA 1, 2013 Bei Sh. 600



[Yaliyomo](#)

- Kanisa kuadhimisha jubili
- Walutheri wafika milioni 6
- NKM Huduma za Jamii aajiriwa
- Jukumu letu kutunza uumbaji
- Kanisa kujenga kituo cha amani Mbagala



Vol. 113, Namba 1, 2013

ISSN 0856 - 1214

Sikiliza

RADIO FURAHA 96.7 FM

Wasiliana nao:

Meneja Radio Furaha FM

KKKT Dayosisi ya Iringa

S.L.P. 511

Iringa, Tanzania

Barua Pepe: rediofuraha@gmail.com

Simu: +255 713 873 151

Kituo bora cha Redio

UPENDO FM RADIO MHz 107.7

Wapo Sokoine Drive

Luther House Gorofa ya Pili.

Mawasiliano:

Mkurugenzi Upendo FM Radio

S.L.P. 13603

Dar es Salaam, Tanzania

Barua Pepe: rediofuraha@gmail.com

Simu: +255 222 124 228

+255 222 139 556

+255 222 124 221

Barua pepe: upendofm@yahoo.com



Uhuru na Amani ni Gazeti la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT). Hutayarishwa na Kitengo cha Mawasiliano, KKKT.

Maoni yaliyomo katika makala zinazochapishwa ni ya mwandishi anayehusika na wala hayawakilishi mawazo ya Kanisa ama mhariri isipokuwa pale ambapo imetamkwa wazi.

Ukiwa na maoni, ushauri, makala au maswali mwandikie:

Mhariri
Uhuru na Amani
S.L.P. 3033
ARUSHA

Barua pepe: elobulu@elct.or.tz
sms kwa Mhariri: 0754-482-285

Fungua Tovuti ya KKKT:
<http://www.elct.org/>

MHARIRI
Elizabeth Lobulu

Yaliyomo

Kanisa lapewa pole

uk. 4

Mchg. Musa awa Askofu

uk. 4

Kanisa lagawa chakula

uk. 5

Askofu Laiser kwaheri

uk. 9

Kanisa laomboleza

uk.16

PICHA YA JALADA:

Mama aliyenufaika na msaada wa chakula katika Dayosisi ya Meru. (picha na rehema samweli/ tcrs). Chini kushoto Mchg. Rachel Axwesso, NKM Huduma za Jamii na Kazi za Wanawake, KKKT. Chini kulia ni Mchg. Martin Junge, Katibu Mkuu wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani aliyeefika Dar es Salaam kuwafariji viongozi na Washarika kwa uharibifu uliotokea Usharika wa Mbagala.

MAONI YA MHARIRI

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) mwaka huu lina adhimisha mwaka wa 50 tangu lianzishwe kutokana na Makanisa saba yaliyokuwepo nchini. Makala mbalimbali zimewekwa katika toleo hili kama sehemu ya mfululizo wa makala zinazoonesha hatua zilizopigwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.

Jubili ni wakati wa kumfanyia Mungu shangwe na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, aliongea kwa furaha hivi karibuni, aliposema 'anamshangaa Mungu' kwa kuwa idadi ya wana-KKKT imeongezeka na kufikia zaidi ya milioni sita mwaka 2012 ikilinganishwa na Washarika 500,000 wa KKKT waliokuwepo mwaka 1963.

Kupanuka kwa kazi ya Injili si kwa idadi pekee, bali hata eneo la kazi linazidi kupanuka. Zile Dayosisi na Sinodi saba zilizopatikana baada ya Makanisa ya Kilutheri kuungana; zimeongezeka na mwaka huu Kanisa lina Dayosisi 22. Kati ya hizo mbili ni mpya kabisa, zitazinduliwa mwezi Mei mwaka huu.

Taswira ya Kanisa na dhamira zinatuelekeza kumhudumia mwanadamu kimwili, kiakili na kiroho kwa njia ya programu na huduma mbalimbali za Kanisa. Kwa eneo hili Kazi ya Kanisa ya kumhudumia mwanadamu mkamilifu inaonekana wazi ikishuhudiwa kwa njia mbalimbali katika jamii ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

Viongozi kwa msaada wa Mungu na Mwongozo wa Kanisa wamejitoa kufanya kazi katika maeneo mbalimbali ili Injili ienee kwa watu wote sambamba na kujihusisha na huduma za kijamii.

Huduma hizo ni kama vile: Kazi za udiakonia, shule, hospitali, visima vya maji, misaada ya maafa au miradi midogo midogo ya ujasiriamali ili kuinua kipato kwa wakulima na wafugaji maskini, kama ufugaji wa nguruwe, ng'ombe wa maziwa na nishati jadidifu ya bayogesi.

Tunamshukuru Mungu kwamba kazi hizi zote na nyingine ambazo hatuwezi kuzitaja hapa zimeweze kana kwa msaada toka kwa Mungu mwenyewe, Washarika waliopokea na kuunga mkono maono ya viongozi wao na Makanisa au Vyama vya Misioni tulivyo na uhusiano navyo ambavyo vilituma wamisionari ili kuanzisha kazi ya Injili Tanzania.

Licha ya changamoto hasa za kiuchumi zinazokabili watu wote na taasisi zote - ziwe za kibinagsi, kiserikali, za ndani na nje ya nchi, je sisi wana KKKT tunatumaini gani pasipo kukubaliana na Paulo alipowaambia Wafilipi: 'Nayaweza yote katika Yeye anitiaye nguvu.' Mambo mengi kwa mwanadamu hayawezekani lakini hayamshindi Mungu. Wakristo tulioitwa kuwa mashahidi na mawakili wa siri zake hatuna budi kwenda na moyo wa kuamini kwamba tunaye mshindi ambaye atatushindia katika mashindano na matatizo katika utume wetu wa kumhudumia mtu mkamilifu. Hongera wana KKKT mnapoolekea kilele cha Jubili ya miaka 50 ya Kanisa letu. Mungu ibariki Afrika. Mungu ibariki Tanzania.

Jukwaa la Viongozi Wakristo Tanzania (TCF) latoa Tamko

Ifuatayo ni sehemu ya Tamko la Pamoja lililotolewa kwa niaba ya Maaskofu 177 walioshiriki katika Mkutano Mkuu wa Dharura wa Jukwaa la Wakristo Tanzania uliofanyika Kurasini, Jijini Dar es Salaam, tarehe 8 Machi, 2013:

"Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia," (Lk.2:14).

1. Utangulizi

Jukwaa la Wakristo Tanzania (TCF) linajumuisha Taasisi Kuu za Makanisa nchini kama ifuatavyo:- Jumuiya ya Kikristo Tanzania - CCT; Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania - TEC; Jumuiya ya Makanisa ya Kipentekoste Tanzania - PCT; Kanisa la Waadventisti Wasabato - SDA (Watazamaji). Wajumbe walifatikari kwa undani juu ya kuzorota kwa mahusiano baina ya Dini mbili za Ukristo na Uislamu nchini Tanzania, pamoja na mauaji na mashambulizi ya viongozi wa dini; na hatua zilizochukuliwa na Serikali dhidi ya uhalifu huo unaotekelawa na Waislamu wachache. Katika taswira hiyo, Kanisa lilitathmini juu ya wajibbu, utume, na sauti yake ya kinabii kwa taifa letu kuhusiana na mambo hayo.

2. Hali halisi ilivyo hivi sasa hapa nchini kwa mtazamo wa Kanisa

Ushahidi wa kihistoria na kimazingira unaonyesha wazi kuwa kwa sasa Kanisa nchini

Kanisa lapewa pole vurugu za kidini nchini

Katibu Mkuu wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), Mch. Martin Junge, aliongoza ujumbe wa watu watatu mwezi Februari mwaka huu kutembelea Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Mbagala, Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam ambalo lilichomwa moto na Waislamu mwaka jana.

Sababu za kuchoma moto Kanisa ni kwa madai kwamba mtoto wa Kikristo alidaiwa kuchafua kitabu cha Korani.

Maaskofu wa KKKT walifika Usharika wa Mbagala tarehe 18 Oktoba 2012 kuwafariji Washarika na Wakristo walio huzunishwa na uharibifu wa mali za Usharika. Maaskofu walitoa tamko ambalo linapatikana kwa kirefu chini ya kichwa: **"Salamu kuhusu uchomaji moto makanisa"** katika tovuti ya KKKT: www.elct.org

Alipotembelea Mbagala, Mchg. Junge, alifuatana na Rais wa Jumuiya ya Makanisa ya Kilutheri Ukanda wa Kati na Mashariki mwa Afrika (LUCCEA), Askofu Dkt. Wakseyoum Idosa na Mchg. Dkt. Musa Filibus - Mkurugenzi wa Missioni na Maendeleo wa Fungamano.

Katika nasaha zao Usharikani Mbagala, Mchg. Junge na Askofu Idosa waliomba Mkuu

Tanzania limo katika kipindi cha mateso ya kimfumo (systematic persecution), kama vipindi vingine 10 vya mateso katika Historia ya Kanisa hapa dumiani.

Pamoja na mateso haya ya kimfumo, tunatambua wazi kuwa wanaotekeleza haya ni kikundi kidogo tu cha Waislamu wa Tanzania, kama wale wengine wa Barani Afrika (k.m. Boko Haram kule Nigeria). Waislamu walio wengi hawafurahii mambo yanayotokea. Wao pia wanaitazamia Serikali kuthibiti hawa wachache wanaochafua dini ya Kiislamu na kuwafanya Waislamu wote waonekane kuwa maadui wa Ukristo, jambo ambalo siyo kweli. Kutokana na hali hiyo, mkutano mkuu wa dharura wa Jukwaa la Wakristo umeyaangalia maeneo makuu yenye migogoro ikiwa ni pamoja na:

2.1. Mgororo wa nani anastahili kuchi-njia kitoweo

Hivi karibuni hapa nchini tume-shuhuduia mgogoro juu ya uchinjaji wa mifugo ambayo nyama yake inapaswa kuuzwa kwa watu wa imani mbalimbali wakiwemo Wakristo na Waislamu. Tunafahamu kwamba sheria ya nchi yetu inaweka bayana juu ya usalama wa nyama hizo kiafya, lakini sheria hailekezi kuwa dini fulani ndiyo waumini wake wanapaswa kuchinja mifugo hiyo. Kwa misingi hiyo Kanisa linatamka kuwa:-

a) Hoja ya dini moja kudai kuhodhi (exclusive right) uchinjaji wa mifugo kwa misingi ya imani

yake ni kinyume cha haki ya uhuru wa kuabudu ambayo amepewa kila mtu ndani ya nchi hii kikatiba katika Ibara 19.

b) Kwa kuwa kuchinja wanyama na ndege ni Ibada kwa Waislamu, Kanisa litambue na kuheshimu jambo hilo. Lakini pamoja na kutambua haki ya Waislamu kujichinjia wanyama na ndege kama Ibada kwao, Wakristo wasilazimishwe kula nyama zilizochinjwa kwa misingi ya Ibada za Kiislamu. Kwa kuwa wananchi wa Tanzania ni wa dini mbalimbali na mila za makabila mbalimbali, tunaitaka Serikali itamke wazi kuwa kila raia ana uhuru wa kufuata imani yake katika suala la uchinjaji.

c) Kuhusiana na jambo hili tunashindwa kabisa kuelewa msimamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine waandamizi wa Serikali.

Wakati wa Serikali ya awamu ya pilis chini ya Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi, ambaye pia ni Muislamu, ulipotokea ugomvi wa mabucha ya nyama ya nguruwe Dar es Salaam, Rais huyu Mstaafu kwa kulinda Katiba ya nchi ambayo aliapa kuilinda, alisema mwenyewe kwa nguvu zote kuwa kila mtu ana uhuru wa kula anachotaka na mtu wa dini moja asimhukumu mtu wa dini nydingine kwa kile anachokula. Baada ya Rais Mstaafu kukemea jambo hili, hali ikawa ya amani na utulivu. Kwa nini Serikali yetu ya sasa inapata kigugumizi kuhusiana na suala zima la nani achinje?

Endelea uk. 17



Baadhi ya waliohudhuria Ibada ya Maaskofu wa KKKT 18 Oktoba mwaka jana kuwapa pole Washarika wa Mbagala.

wa Kanisa na Washarika wawe na moyo wa uvumilivu na wala wasifikirie kulipiza kisasi licha ya kuwepo madhara na uharibifu mkubwa wa Kanisa lao.

Jukwaa la Viongozi Wakristo Tanzania nalo iliunga mkono KKKT kwa kutoa tamko lao

ambalo pamoja na mambo mengine, liliomba Serikali ichukue hatua za dhati kuhakikisha wahalifu wanaotaka kuharibuu amani wanachukuliwa hatua haraka. *Soma Tamko hapo juu lililotolewa hivi karibuni.*

Kanisa lagawa chakula kusaidia watu wasife njaa

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limetoa msaada wa chakula kwa watu walio katika maeneo ya ukame Kaskazini mwa Tanzania ili wasife njaa.

Tani 264 za mahindi na tani 10 za mbegu ya mtama zimesambazwa katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha kati ya Januari na Machi mwaka huu.

Serikali ilitangaza kwamba wilaya 50 zilizopo Kaskazini mwa Tanzania zimekumbwa na uhaba mkubwa wa chakula kutopteka na ukame, upungufu wa mvua na kwa kuwa wakulima walio wengi wanaendesha kilimo kinachotegemea uwepo wa mvua.

Naibu Katibu Mkuu Mipango na Maendeleo KKKT, Bw. Mallumbo William Mallumbo alisema hivi karibuni kwamba licha ya kuwapatia msaada wa chakula, waliokumbwa na ukame pia walipatiwa mbegu za mtama ambazo hustahimili hali ya ukame kwa kuwa ziko dalili kwamba ukame utaendelea kama ilivyokuwa mwaka uliopita.

Washirika wa KKKT kupitia shirika la ‘ACT-Alliance’ walichangia Dola 234,954.34 ili kuwezesha Kanisa kugharamia chakula hicho. Michango ilitoka Kanisa la Sweden waliopta Dola 71,776.34; Kanisa la Kilutheri la Bavaria (Dola 77,640); ‘Finnish Evangelical Mission’ Dola 77,538 na Marekani kupitia Shirika la ‘Wider Church Ministries’ (Dola \$ 8,000).

Kwa maelezo zaidi fungua tovuti ya KKKT: www.elct.org



Baadhi ya waliopokea chakula cha msaada Dayosisi ya Pare wakikiweka katika vifungasho. (picha na rehema samweli/ tcrs)

KKKT yateua NKM Huduma za Jamii



Mchg. Rachel John Axwesso,
Naibu Katibu Mkuu Huduma za Jamii
na Kazi za Wanawake, KKKT.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) limemteua Mch. Rachel John Axwesso kuwa Naibu Katibu Mkuu Huduma za Jamii na Kazi za Wanawake kuanzia Januari Mosi kuchukua nafasi iliyoachwa na Mch. Sabina Lumwe aliye maliza kipindi chake Desemba 2012.

Mch. Axwesso aliyezaliwa Mbulu Desemba 22, 1964, alihitimu Shule ya Msingi Endoji iliyopo Dongobesh na kuijunga na Shule ya Wasichana Tabora alikosoma Kidato cha Kwanza hadi cha Sita ambapo alimaliza masomo hayo mwaka 1990.

Kabla ya kazi yake mpya Mch. Axwesso alikuwa Mkufunzi katika Shule ya Udkonia Faraja iliyopo Wilayani Hai, Mkoani Kilimanjaro.

Ana Shahada ya Uzamivu katika Theolojia (M The) aliyopata Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA) 2003 na Shahada ya Mambo ya Dini (BD) ya chuo cha TUMA mwaka 1997.

Baada ya kuhitimu shahada ya kwanza TUMA alibarikiwa kuwa Mchungaji katika Usharika wa Karatu mwaka 1998 na amehudumu katika Sharika mbalimbali Wilayani Hai, hasa Lyamungo Kati (1998 - 2012). Pia aliwahi kuwa Mchungaji wa Hospitali ya Kilutheri Karatu (Chaplain) Mkoani Manyara 1990 - 2001. Ameolewa na John Axwesso na wamejaliwa watoto wanne; wasichana 3 na mvulana 1.

Kukomesha mauaji ya viongozi wa dini ya Kikristo • CCT yaomba hatua zaidi zichukuliwe

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Askofu Peter Kitula, aliiomba Serikali ichukue hatua zaidi ili kukomesha mauaji ya viongozi wa dini ya Kikristo. Hayo yalismwa na Mwenyekiti huyo wa CCT, hivi karibuni jijini Arusha.

Alisema wapo mashehe wa Kiislamu wanaosikika hadharani wakiwaambia waumini wao: “mkiona Kadinali, Askofu, Mchungaji au Padri ua. Na hofu inaingia kwa kuwa mauaji yameshaanza kutokea Buselesele, Wilaya ya Geita na Zanzibar,” alisema.

Uchinjaji wa wanyama

Kuhusu suala la kitoweo, Askofu Kitula alisema inaelekeea kwamba suala la kuchinja wanyama kwa ajili ya kitoweo ni la kiibada. Lakini alitaka Serikali isilazimishe watu ambao hawapendi kujihusisha na wanyama wanaochinjwa kiibada. Baadhi ya watu wanapenda nyama inayouzwa katika maduka ya vitoweo ichinjwe na mwislamu; alisema na kuongeza kuwa mahali ambapo Mkristo amechinja waislamu wamelazimisha kitoweo hicho kisusiwe au wamediriki kukiharibu.

Laiser shujaa, shahidi wa Injili - Maaskofu

Askofu Dkt. Thomas Olmorijoi Laiser, aliyekuwa Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini Kati ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), aliaga dunia 7 Februari 2013 akiwa Hospital ya Kilutheri ya Arusha (ALMC) na kuzikwa Usharika wa Mjini Kati Arusha tarehe 15 Februari. Maaskofu karibu wote wa KKKT walihudhuria. Mionganoni mwa waombolezaji alikuwepo pia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, ambaye alifuatana na ujumbe mzito wa viongozi wa Serikali na Chama cha Mapinduzi.

Ifuatayo ni sehemu ya salamu za Rais alizozitoa siku ya mazishi:

"Kwa niaba yangu binafsi na, kwa niaba ya Serikali na wananchi wa Tanzania niruhusuni, kwa mara nyingine tena, nitoe mkono wa pole na rambirambi kwako wewe, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, kwa Maaskofu, Wachungaji na Washarika wote wa KKKT, Dayosisi ya Kaskazini Kati kwa msiba huu mkubwa uliowakuta.

"Poleni sana kwa kuondokewa na kiongozi wenu shupavu wa kiroho na aliyetao mchango mkubwa kwa uhai na ustawi wa Kanisa lake na maendeleo ya watu.

"Aidha, ninatoa pole nyingi sana kwa mke wa marehemu, Mama Maria Luka Laiser, pamoja na familia yake kwa kuondokewa na mume, baba, babu, kiongozi na mhimili muhimu wa familia. Naelewa uchungu na majonzi mlionayo. Napenda kuwashakikishia nyote kuwa msiba huu ni wetu sote. Uchungu wenu ni wetu na majonzi yenu ni yetu pia.

"Kifo cha Askofu Dkt. Thomas Laiser kimetokea wakati mchango wake ulikuwa bado unahitajika sana. Nilifahamiana na Askofu Dkt. Laiser kwa miaka mingi, tangu nikiwa Waziri mpaka sasa. Nilimfahamu kuwa ni kiongozi wa kiroho mahiri na muadilifu. Pia alikuwa kiongozi hodari, mpenda maendeleo ya jamii na wa kutumainiwa sana na jamii. Alitoa mchango mkubwa sana kwa Kanisa lake la KKKT na kwa maendeleo ya waumini wake na wananchi wote waishio katika Dayosisi yake ya uongozi na kwingineko.

"Matunda ya jithada kubwa alizozifanya katika kuwashudumia waumini na wananchi wa Dayosisi ya Kaskazini Kati na Watanzania kwa ujumla zinajieleza zenyewe. Shule, vyuo, zahanati, vituo vya afya, hospitali, miradi ya maji na mambo mengi aliyoyafanya ni ushahidi wa ukweli huu ninao uzungumza. Watu wengi kutoka ndani na nje ya Dayosisi hii wamenufaika, wananufaika na wataendelea kunufaika na huduma zilizopatikana kwa ubunifi na jithada za marchemu Askofu Thomas Laiser. Daima atakumbukwa kwa mambo mengi mazuri aliyolifanya Kanisa lake, waumini wake na wananchi wa Tanzania kwa ujumla.

"Marehemu Askofu Laiser alikuwa mpenda watu. Alihubiri upendo, umoja na amani kwa


siasa. Sote tuige mfano mzuri wa hayati Askofu Laiser, wa watu kuishi pamoja kwa upendo, amani na ushirikiano licha ya tofauti zao.

"Najua wote sisi tungependa mtu mwema kama huyu aendeelee kuwa nasi ili tuzidi kunufaika na busara zake, mchango wake, uongozi wake na utumishi wake. Lakini, Mwenyezi Mungu, ambaye ndiye muweza wa yote, amempenda zaidi na kuamua kumchukua.

"Hatuwezi kumlaumu wala kumsiktitika kwani daima tunatambua kuwa kazi yake haina makosa. Hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa muda na nafasi aliotupatia ya kuishi na Askofu Laiser hapa duniani na kunufaika na mchango wake adhimu. Kilicho wajibu kwetu kufanya ni kuzidi kumuomba Mwenyezi Mungu ampokee marehemu wetu, ampe mapumziko mema na amjalie pepo. Amina."



Rais Mstaafu Benjamin Mkapa, Rais Kikwete, Rais Mstaafu Ali Hassan Mwinyi na Waziri Mkuu Mstaafu Edward Lowasa wakiwa katika mazishi ya Askofu Laiser.



Mch. Solomon
Masangwa, Kaimu
Mkuu wa Dayosisi
ya Kaskazini Kati.

1963



2013

Historia fupi ya KKKT

Dkt. Martin Luther

Muasisi wa Kanisa ya Kilutheri Duniani, Mchg. Dkt. Martin Luther, alianzisha "Matengenezo ya Kanisa" jijini Wittenberg, Ujerumani mwaka 1517. Watu waliofua mafundisho ya Luther wakaitwa "Walutheri".

Mafundisho ya Dkt. Luther yaliwawutia wengi kwa uamsho wa kipekee na hasa alipowafundisha kwa ufasaha juu ya msingi mkuu wa wokovu kama yasemavyo Maandiko Matakatifu (Biblia). Mikazo ilikuwa mitatu: imani tu (Sola Fide), neema tu (Sola Gratia), na Neno tu au Kristo tu (Sola Scriptura, Sola Christus).

Baada ya hapo Kanisa la Kilutheri limeenea kote duniani kuitia wamisionari mbalimbali na vyama vya Injili.

Kwa takwimu za mwaka 2011 Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD), Walutheri duniani wamefikia watu milioni 70. Ufikapo 2017 tutaadhimisha miaka 500 ya Kanisa la Kilutheri Duniani.



Nembo ya
Martin Luther

Makanisa saba ya KKKT

Kanisa la Kilutheri liliingia nchini mwetu kwa mara ya kwanza mwaka 1887 ambapo Wamisionari kutoka Berlin III walifika Uzaramo-Uluguru na kuanzisha kazi ya Injili.

Kati ya mwaka 1887 na 1939 wamisionari walifika kwenye maeneo mbalimbali ya nchi yetu kama ifuatavyo:

- Wamisionari wa Berlin III walianzisha Kanisa la Uzaramo-Uluguru 1887.
- Wamisionari wa Berlin I walianzisha Kanisa la Ubena-Konde 1891.
- Wamisionari wa Berlin III walianzisha Kanisa la Usambara-Digo 1891.
- Wamisionari wa Leipzig walianzisha Kanisa la Kaskazini 1893.

- Wamisionari wa Bethel walianzisha Kanisa la Buhaya 1910.
- Wamisionari wa Leipzig na Wamisionari wa Kichaga walianzisha Kanisa la Iramba-Turu 1911.
- Wamisionari wa Sweden walianzisha Kanisa la Mbulu 1938/ 39.

Wamisionari walifika maeneo yaliyotajwa awali walianzisha makanisa yanayojitegemea na baadaye baadhi ya majina ya makanisa hayo yilibadilishwa kulingana na wakati na kukua kwa huduma. Na ilipofika tarehe 19 Juni 1963 makanisa hayo saba ya Kilutheri yaliyokuwepo nchini yaliungana na kuunda Kanisa moja la KKKT - Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania.



Pata
nakala ya
Kitabu cha
"Tumwabudu
Mungu Wetu"
kutoka
Usharikani
kwako.

Kanisa kuadhimisha jubili ya mwaka wa 50 mwezi Juni

• Mkuu wa KKKT amshangaa Mungu kwa baraka na kukua kwa Kanisa

Akiongea kuhusu kiashirio cha ongezeko la idadi ya Washarika, Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Alex Malasusa anasema:

"KKKT ilipoanzishwa ilikuwa na Wakristo wapatao 500,000 na katika mwaka wa Jubili tuna wakristo zaidi ya milioni sita; huu ni ukuaji mkubwa

nasi tuna kila sababu ya kumshukuru Mungu kwani ndiye mwenye kulijenga na kulisilishi kundi lake."



Picha ya Maktaba ni ya baadhi ya wajumbe wa Mkuu wa KKKT wakifutilia kwa makini mada ilipokuwa ikitolewa.



Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Theologia na Maadili, KKKT walipokutana hivi karibuni jijini Arusha. Walijadili majukumu ya Kanisa katika utume wake.

1963



2013

Idadi ya wa Walutheri Tanzania yafikia m 6

Washarika wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) hadi Januari 2012 wamefika 6,139,879 ukilinganisha na idadi ya washarika 5,825,312 mwaka 2011 ambalo ni ongezeko la watu 314,567 kwa mujibu wa taarifa toka kwa Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa.

Alisema hivi karibuni kwamba idadi ya Washarika ni ongezeko la asilimia 5.4 ikilinganishwa na mwaka 2011. Takwimu za Washarika wa KKKT kwa kipindi cha miaka michache iliyopita ni kama ifuatavyo: mwaka 2007 walikuwa 4,632,480; mwaka 2008 - Washarika 4,956,731; 2009 - Washarika 5,303,727; 2010 - Washarika 5,601,217 na Januari 2011 walikuwa Washarika 5,825,312.

Hatua zilizopigwa na Kurugenzi ya Kazi za Wanawake

Na Rachel Ramadhani

Utangulizi

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) kwa kutambua

KKKT ni la tatu duniani

KKKT ni Kanisa la tatu kwa ukubwa duniani katika familia ya makanisa 145 ya Kilutheri baada ya Kanisa la Sweden na lile la Ethiopia liitwalo Mekane Yesus. Tena ni Kanisa la pili kwa ukubwa barani Afrika baada ya lile la Ethiopia.

Mahudhurio makubwa

KKKT ni moja ya makanisa yanayoongoza nchini kwa watu wengi kuhudhuria Ibada makanisani.

Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira chapanuka

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dkt. Alex Malasusa, ambaye pia ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA), tarehe 3 Machi 2013 alizindua rasmi Kituo cha Mbeya kuwa sehemu ya TUMA.

Katika hatua ya kupandishwa hadhi ya Chuo cha Kilutheri cha Ualimu Mbeya kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira, tarehe 8 Oktoba

Viongozi wake wa kwanza walikuwa:

Bibi Veronica Swai - Mwenyekiti; Bibi Phoebe Mnande - Makamu Mwenyekiti; Bibi Kristolumba Mzengi - Mwandishi na Bi Janet Luvanda - Katibu wa Idara.

Wakati huo Idara ilijulikana kama *Umoja wa Wanawake* na wajumbe wake walikuwa Makatibu/ Waratibu wa Wanawake katika Dayosisi/ Sinodi za KKKT. Umoja huo uliandaa *"Mwongozo wa Kazi"*. Madhumuni ya umoja yalikuwa yafuatayo: Kwanza ni kuwaunganisha wanawake wa KKKT, kujenga na kuimarisha imani yao katika Yesu Kristo, kwa kujifunza na kutenda kama Neno la Mungu linavyoagiza.

Pili Idara ya Wanawake, kama kiungo cha Kanisa, inahimiza huduma ya Injili katika Kanisa; ushirikiano wa kindugu na matendo ya upendo katika Kanisa na jamii. Pia inawapa nafasi wanawake wawze kutumia talanta walizonazo ili kumtumikia Mungu.

Kazi za Idara zilikuwa zifuatazo:

- Kuhamasisha Dayosisi kuwa na Idara za Wanawake zinazotambulika Kikatiba.

Endelea uk. 13

Tunakaribisha maoni

Ndugu Msomaji,

Tunakaribisha picha na makala kwa kifupi kuhusu mada hii: *Je, hatua gani KKKT imepiga kwa kipindi cha miaka 50 tangu liwe ni Kanisa moja la Kiinjili la Kilutheri Tanzania?* Maoni hayo yatawekwa katika toleo maalumu la Gazeti la *Uhuru na Amani* la mwezi Juni. Barua pepe: elobulu@elct.or.tz

Mhariri.



Idadi ya wajumbe wanawake katika vikao vya maamuzi inaongezeka siku hadi siku kama inavyoonekana pichani juu wakati wa Mkutano Mkuu uliopita. Idadi ya Wachungaji wanawake imefikia 200 mwaka 2013 kati ya Wachungaji wapatao 2,000 KKKT.

Kwaheri Askofu Laiser



Marehemu Askofu Dkt. Thomas Olmorijoi Laiser

1945 - 2013



Baadhi ya Maaskofu toka
ndani na nje ya Tanzania
waliohudhuria mazishi ya
Askofu Laiser.

Mahubiri ya Mkuu wa KKKT

Askofu Dkt. Alex Malasusa

Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, akihubiri siku ya mazishi ya Askofu Dkt. Thomas Laiser alisoma Neno toka Warumi 8:33 - 36 na kufanua kwamba hakuna mwanadamu awezaye kuzuia mapenzi ya Mungu yasitimie. Ndiyo maana Ayubu anasema Bwana ametoa na Bwana ametwaa jina la Bwana lihimidiwe. Endelea kusoma:

“Kwa wakati huo Rumi wapo watu walioishi

bila kuamini kuna kifo na walidhani maisha yalifikia kikomo chake bila kuongozwa na Mungu. Hata katika maisha ya watu leo *wapo wanaoishi kama vile wame maliza safari*. Hawapendi Ibada wala kukumbushwa kuhusu roho zao.

Mungu ameweka mwili na moyo uliobebwa na mwili na katika moyo uko uzima wa milele. Paulo anasema ‘*maisha na uzima uko kwa Mungu*’ ndio maana madaktari wameushughulikia mwili wa

marehemu lakini Mungu amemchukua. Tukumbuke watakao shinda vita ya kiroho ndiyo watakaofika mbele za Mungu.

Kila ulipomtembelea alipokuwa mgonjwa, Askofu Laiser, aliomba afanyiwe sala. Alikuwa kiongozi aliyetamani *watu wote wautafute uso wa Mungu na kujiveka sawa ili kuweza kuurithi uzima wa milele*. Na sisi tunakumbushwa kujijandaa ili kuurithi uzima wa milele.

Wanadamu tumepewa muda mfupi wa kuishi duniani ili *tuweze kumpa Mungu mioyo yetu aitawale na kutupatanisha nafsi zetu naye* kama Neno lisemavyo: ‘*Tafuteni*

Endelea uk. 11



Mkuu wa KKKT
Askofu Dkt. Alex Malasusa
aliongoza Ibada ya mazishi.

Salamu za Maaskofu KKKT

Zifuatazo ni salamu zilizotolewa na watu mbalimbali:

Askofu Japhet Mengele

KKKT Dayosisi ya Kusini

Kifo cha Askofu Dkt. Thomas Laiser kitumike kuenzi na kutunza mambo mema aliyoafanya kwa manufaa ya Dayosisi ya Kaskazini Kat, KKKT na Watanzania kwa kuwa alitoa mchango mkubwa wa kuinua Watanzania kwa miradi ya maendeleo na kijamii. Sasa mjiulize je, na ninyi mtafanya nini kumuenzi? Baba Askofu Laiser alikuwa mtetezi wa watu na Kanisa. Washarika mijipe moyo na kuzidi kumwomba Mungu kutokana na pengo aliloliacha.

Askofu Jacob Mameo Ole Paulo

KKKT Dayosisi ya Morogoro

Askofu Laiser alisifika kwa maneno yake ya hekima na alikuwa mtu mwenye sifa nzuri za uongozi katika jamii. Alipenda watu na alipenda wanyama pia. Ndiyo maana mifano katika kauli zake, hakuacha kutaja wanyama. Naomba Mungu aweze kumnyanya kiongozi mwingine atakayekuwa jasiri na anayependa kusema kweli bila hofu kama alivyo kuwa Askofu Laiser. Yalipotokea masuala magumu ya kitaifa; Kanisa lilimtafuta Askofu Laiser maana ye ye aliwa, ‘akikanyaga amekanyaga, hata kama ni mkaa wa moto haondoi mguu’. (Jambo ambalo lilifanya

watu wacheke. Na akiwa katikati ya salamu akabadili lugha na kuanza kumsemesha mjane Kimasai maneno yaliyotafsiriwa kwamba:) Sasa wewe ndiyo baba na ndiyo mama wa familia; vaa viatu vipyaa maadamu umebacki na watoto wa kiume na wa kike. Endeaza kazi za kilimo na mifugo kwa maendeleo ya familia na uombe Mungu kwa kila jambo ili Mungu akuwezeshe. Alisoma Yohana 14: 1-2 “*Msifadhaike miyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali.*”

Askofu Dr. Israel-Peter Mwakyolile

KKKT Dayosisi ya Konde

Kanisa limepoteza shujaa aliyejewa mtetezi wa wanyonge hasa wafugaji walipopokonywa ardhi yao na watu walio na uwezo kiuchumi. Pole mjane, Mama Mary Laiser, kwa kazi kubwa ya kumtunza Askofu alipokuwa mgonjwa nakuombe Mungu Shetani asikuletee majaribu. ‘*Bwana Yesu ni Bwana wa wajane na baba wa yatima*’. Faraja ya Neno lilitoka Warumi 8: 31 -39.

Nilipokea taarifa ya msiba nikiwa Ujerumani, hivyo naleta salamu za pole toka uongozi wa Kanisa la Kilutheri Bavaria, Ujerumani.

upendo wa Bwana Yesu:

Askofu Laiser alihubiri kwa vitendo na alikuwa balozi na shahidi mzuri wa Yesu Kristo bila kujihurumia ila alihakikisha Injili ya Kristo inamfikia kila mtu. Yeye alikuwa mtu makini na mara alipotambua jambo fulani ni la Bwana Yesu alilishikilia na hakuna aliymrudisha nyuma.

Umati mkubwa uliohudhuria mazishi unaonesha jinsi watu walivyopenda ila Mungu amempenda zaidi. Kifo hiki kinazungumza nasi kwamba mimi na wewe sasa tuijweke tayari na kwamba iko siku sote tutakufa.

Lakin siku nikifa watu watasema nini juu yangu? Je Mungu atasema: ‘*Njoo wewe ni mwanangu kwa kuwa umefua mavazi yako na kuyafanya meupe katika damu ya Mwana-Kondoo,* (Ufunuo 7:9-17).’

Balozi wa Kristo

Inatoka uk. 10

kwa bidii kuwa na amani na watu wote.

Waraka kwa Waebrania unasema: ‘*Hapa duniani hatuna mji udumuo*’. Tuutafute utakatifu ili tuweze kukutana na Bwana Yesu atukaribishe tuwe pamoja naye. Tusitamani tu maendeleo ya kibinadamu bila kujali roho zetu bali tuhakikishe ‘*wote wanaupata*



Picha ya maktaba - Kushoto ni Rais Jakaya Kikwete alipokuwa akitoka Ukumbi wa Mikutano AICC 2006 akiwa na marehemu Askofu Laiser (katikati aliyevea msalaba) mara baada ya Rais kufungua baraza la Idi.

Salamu za LMC

Askofu Mwakyolile ambaye pia ni Mwenyekiti wa Lutheran Mission Cooperation (LMC) alisema: Askofu Laiser alikuwa na uwezo wa kuonesha msimamo unaolitambulisha Kanisa mbele ya vikao na makanisa rafiki. Yeye alipenda kusisitiza kwamba tuheshimiane katika tofauti tulizonazo. Kwa jinsi hiyo Kanisa limeondokewa na mtu muhimu. Naomba Mungu amnyanyue mtu mwininge wa aina hiyo. “*Heri wafu wafao katika Bwana ... maana matendo yao yafuatana nao*,” (Ufunuo 14: 13)

Askofu Amon Kinyunyu

KKKT Dayosisi ya Dodoma

Nilitambua kwamba Askofu Laiser anareshimiwa na watu kwa vile katika kazi ya kueneza Injili katika jamii ya Wamasai waliopo Dodoma; wenyeji walikuwa wakiwaliza Wachungaji: ‘*wewe umetoka Kanisa la Laiser?*’ Na pindi watumishi wa Kanisa wakisema *wanatoka kwa Laiser*, walipokelewa vizuri na kazi ikaweza kusonga mbele. ‘*Niite nami nitakuitika*.’ (Yeremia 3: 19b).

Mkuu wa KKKT

Askofu Dkt. Alex Malasusa

Askofu Laiser alikuwa ni shujaa wa imani na mtu aliyesimama katika nafasi yake. Washarika mjiandae kwa ‘*kutengeneza mambo yenu*’ kama Neno lisemavyo katika Isaya 38: 1.

Askofu Mteule Lucas Mbedule

KKKT Dayosisi ya Kusini

Mashariki

Alipomfufua Lazaro Bwana Yesu alisema: ‘*Yeye aniaminie ataishi hata kama amekufu bado ataishi*’ na ndivyo tunavyo amini kufuatia kifo cha Askofu Laiser. Historia yake inaonesha hakuwa mzee sana. Lakini usiangaliwe wingi wa miaka, bali ni nini alichofanya. Washarika mliaoachwa muungane wote ili mjenge jamii moja ya wana-Dayosisi wote yenye heshima mbele za Mungu na jamii. Daima muombe na kuijeweka mikononi mwa Mungu.

Askofu Michael Adam

KKKT Dayosisi Mkoani Mara

Nakumbuka kipawa chake wakati wa vikao aliyowezza kueleza mambo magumu kwa lugha nyepesi. Wana-Dayosisi mpange namna ya kuendeleza yote aliyoafanya kazini na mahali pengine baada ya *kutwaliwa kwake*.

Muendelee kuwasaidia na kuwafariji mjane na wanafamilia wengine. Mungu wa baraka aendelee kuwa na Dayosisi ili yote yawe baraka.



Mama mjane Mary Laiser (wa pili kushoto) akitoa heshima za mwisho. Baadhi ya waombolezaji (Kulia) wakati wa Ibada fupi katika Hospitali ya 'Arusha Lutheran Medical Centre' (ALMC).

Salamu mbalimbali

Askofu Mstaafu Elinaza Sendoro

Nilimfahamu Askofu Laiser tangu 1978 niliposafiri pamoja naye kwenda Wuppertal, Ujerumanili ili kujumuika na jopo kujadili jinsi ya kuunda taasisi iliyokuja kujulikana kama '*United Evangelical Mission*' (UEM). Alikuwa ni rafiki wa karibu wa familia. '*Na amani ya Mungu ipitayo akili zote, itawahifadhi miyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu,*' (Wafilipi 4: 7).

Askofu Mwamba Sumaili Mkuu Kanisa la Kilutheri Kongo

Binadamu anatoka katika maisha haya kwa njia ya kifo. '*Kanisa liko katika hali ya ujane na ukiwa*' lakin Washarika mkumbuke mambo mema yaliyofanywa na marehemu wala msiyasahu kama ilivyo kawaida ya wanadamu. **Nukuu:** Wafilipi 2: 1 – 3.

Salamu za Kanisa la Anglicana Askofu Mkuu Valentine Mokiwa

Kwa niaba ya Kanisa la Anglicana Tanzania; Baraza la Makanisa Afrika (AACC) na kwa niaba ya Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglicana Duniani nawapa pole. Askofu Laiser aliakuwa ni '*Askofu wetu sote*', aliakuwa jasiri na kila alipozungumza hakuchanganya unafiki. Katika maisha yake aliakuwa mtetezi wa haki za wanyonge. "*Lakini mimi najua ya kuwa Mteteaji wangu yu hai, na ya kuwa hatimaye atasimama juu ya nchi,*" (Ayubu 19: 25). Alikuwa mtu wa udhubutu na aliakuwa kama mshumaa ulioongeza nuru.

Alifanya yale aliyoaamini na hata pale alipokosea mambo hayo yote yatabaki katika kumbukumbu kwamba alipenda kuwaletea watu maendeleo. Yeye alimtazama Kristo na kwa hiyo tulioabaki *tutulie maana Mungu yu pamoja nasi*. Inabidi tutimize aliyouchia ili

kazi ya Injili iendelee mbele.

Salamu za Kanisa Katoliki Askofu Mkuu Josephat Lebulu

Kwa niaba ya Baraza la Maaskofu wa Kanisa Katoliki Tanzania (TEC), nawapa pole Wakristo wote, mjane, wanafamilia na wafiwa wote. Nitamkumbuka sana Askofu Laiser hasa kwa jinsi tulivyoshirikiana katika Umoja wa Madhehebu ya Kikristo Mkoani Arusha. *Anayekufa katika imani ataufikia uzima wa milele*, kama alivyoahidi Bwana Yesu kutowatupa *watakao mwamini na kumjia*, (Yohana 6: 36 -37). Askofu Laiser alitoa mchango mkubwa katika jamii kwa kuwaendeleza watu kiroho, kiakili na kimwili. Askofu hakuvumilia uonevu bali aliakuwa na ari ya kuotesha kinachokuzaha kiki na kubomoa misingi iletayo ukandamizaji.

Alipenda pawepo mshikamano wa kijamii na kwa hiyo alipenda kuharibu sumu au fikra au kauli za utengano.

Alipenda kutafuta dawa ya kuponya na kutoa kauli ya kuangamiza adui wa haki ili kudumisha umoja katika jamii. "*Angalia nimekuweka leo juu ya mataifa na juu ya falme ili kun'goa, na kubomoa na kuharibu na kuangamiza ili kujenga na kupanda*," (Yeremia 1: 10).

Askofu Zakaria Kahuthu, Kanisa la Kilutheri Kenya

Nilimfahamu Askofu Laiser kwa muda mrefu. Nawapa wafiwa na Washarika pole kwa kuondokewa na mtu waliyempenda.

"Kwa maana kama tukiishi, twaishi kwa Bwana au kama tukifa twafa kwa Bwana. Basi kama tukiishi au kama tukifa, tu mali ya Bwana," Warumi 14: 8 – 9.

Salamu za Mwenyekiti wa CCT Askofu Peter Kitula

Askofu Laiser aliakuwa shujaa, nabii na

kiongozi mahiri aliyetoa mchango mkubwa kwa Kanisa na jamii kwa jumla.

Alitumika CCT na Jukwaa la Viongozi wa Kikristo Tanzania. Ameondoka wakati ambapo sauti yake ya kinabii inahitajika hasa kwa sasa tunavyo shuhudia dalili za kuvunjika kwa amani, mshikamano, utilivu na umoja wa kitaifa. *Atakaye amini Neno langu yu na uzima wa milele*', (Yohana 6: 47).

Viongozi wengine waliota salamu ni Askofu Gary Wollersheim toka Sinodi dada ya 'North Illinois' ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKK) Marekani na Mkurugenzi wa Misioni ya Leipzig, Mch. Tobias Kruger, amba walikuja Tanzania kwa ajili ya mazishi hayo.

Askofu Gary Wollersheim Kanisa la Kilutheri Marekani

Nilimfahamu Askofu Laiser kwa zaidi ya miaka 20 aliposhiriki Ibada ya kuniweka wakfu kuwa Askofu mwaka 1988 huko Illinois. Natoa pole kwamba waombolezaji mjipe moyo kwa kuwa '*Wakristo wana mtumaini Bwana katika ufufuko*.' Askofu Laiser aliakuwa baba yangu wa kiroho na nilijifunza mambo mengi toka kwake. Kila mara nilipopata changamoto nilimkumbuka. "*Uwe hodari na moyo wa ushujaa; usiogope wala usifadhaike; kwa kuwa Bwana Mungu wako yu pamoja nawe kila uendako*," (Yoshua 1: 9).

Mch. Dkt. Musa Filibus Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani

Tumepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Askofu Thomas Laiser. Tunajumuika nanyi kwa kuwaombea na kuwakumbuka.

Hata sasa anapozikwa mjue hamko peke yenu bali tuko pamoja nanyi. Utumishi wa Askofu Laiser katika Kanisa, alilolitumikia hadi dakika ya mwisho, unaonesha alivyoishi Injili ya Yesu Kristo si kwa mahubiri bali kwa matendo. Na sisii 'sote tuliobakia' tuige mfano huo. "*Msifadhaike miyoni mwenu; mniamwamini Mungu, niaminini na mimi*," (Yohana 14: 1).

1963



2013

Wanawake

Inatoka uk. 8

- Kuwafundisha wanawake kazi za mikono, ufundi na ujasiriamali ili waweze kufanya biashara ndogo ndogo kuinua kipato cha familia na Idara kwa njia ya *kambi za wanawake* kwa ajili ya kazi hizo. (Kambi zilidumu kwa mwezi mmoja mpaka miezi mitatu).
- Kuwapa Wanawake mafunzo mbalimbali katika vikundi, kama: *Mafunzo ya Ndoa na Unyumba, Malezi ya Watoto, Afya, Lishe, Masomo ya Biblia na Masomo ya Uongozi.*
- Mambo mengine ni pamoja na: Kazi za Udiakonia, kama vile kuwafariji na kuwasaidia wagonjwa, wasio jiweza, wajane na yatima. Kuongoza *Maombi ya Dunia* kila mwaka.
- Kuanzisha vituo vya Elimu ya Awali (Chekechea).
- Kufundisha *Shule ya Jumapili* kwa

JOKUCO tawi jipya la Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira

Kuzinduliwa rasmi kwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Josiah Kibira (JOKUCO) kumeongezea matawi ya Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira (TUMA) ambayo sasa yamefika sita. Ibada na sherehe ya kufana ilifanyika Bukoba Januari 12 ambapo Mkuu wa Mkoa wa Kagera Kanali mstaaful Fabian Massawe alikizindua chuo hicho.

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ambaye pia ni Mkuu wa TUMA, Askofu Dkt. Alex Malasusa, aliongoza Ibada ambayo ilihudhuriwa pia na Makamu Mkuu wa TUMA, Mch. Prof. Joseph Parsalaw, Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Brighton Killewa, na mwenyeji wao Askofu Elisa Buberwa, Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini Magharibi.

Watu wapatao 900 waliohudhuria.
Dkt. Malasusa alisisitiza vyuo vikuu

kufuata Mwongozo ulioandaliwa na Kitengo cha Elimu ya Kikristo.

Mabadiliko ya muundo

Kati ya miaka ya 1995 - 2010 Ofisi Kuu ya KKKT ilibadilisha muundo wa uongozi na utawala wa Idara zake. Katika mabadiliko hayo Idara ya Wanawake ikaitwa: *Kurugenzi ya Programu za Kazi za Wanawake na Watoto*. Na iliwekwa iwe *Kitengo cha Idara ya Huduma za Jamii na Wanawake*.

Viongozi wa Kurugenzi ya Programu za Kazi za Wanawake na Watoto, KKKT tangu 2010 hadi taarifa ilipokuwa inatolewa Machi 2013 ni hawa wafuatao: Bibi Monica Ngavatula - Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wanawake KKKT; Bibi Mary E. Laiser - Makamu Mwenyekiti; Mch. Joyce Kibanga - Mwandishi wa vikao na Bibi Rachel Ramadhani, Mkurugenzi wa Programu ya Kazi za Wanawake na Watoto.

Kurugenzi iliboresha "*Mwongozo wa Uongozi*" na kujikita katika programu au majukumu yafuatayo:

- Mafunzo ya Uongozi.
- Mafunzo ya ushauri wa Kichungaji.
- Mafunzo ya ujasiriamali.

vya Kanisa visimamie maadili mema ili kutoa viongozi walio hodari na waadilifu katika jamii.

Vyuo vikuu vishiriki vya TUMA ni: Chuo Kikuu Kishiriki cha Josiah Kibira; Makumira, ambayo ni kampasi kuu ya TUMA; Chuo Kikuu Kishiriki cha Iringa; Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam; Chuo Kikuu Kishiriki cha KCMC na Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano Moshi. Kwa maelezo zaidi fungua tovuti: www.makumira.ac.tz

SEKOMU

Tangu Oktoba 2012 Chuo Kikuu Kishiriki cha Sebastian Kolowa kinajitegemea na kinaitwa *Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Sebastian Kolowa* (SEKOMU).

- Mradi wa nguruwe.
- Maombi ya Dunia.
- Shule ya Jumapili.
- Haki za binadamu.
- Maandalizi ya Kituo Cha Wanawake.
- Mafunzo kwa Wachungaji wanawake Mafunzo kwa Wachungaji na Watheolojia wanawake hufanywa wakati fedha ya shughuli hiyo inapopatikana. Makongamano manne yamekwisha fanyika kwa ajili ya wachungaji wanawake tangu programu hiyo ilipoanza kwa udhamini wa Fungamano la Makanisa ya Kilutheri Duniani (FMKD) tangu 1999. Tunatarajia Kongamano lijalo litakuwa 2013.

Mikutano mbalimbali

Kufuatana na Mwongozo wa Kurugenzi, wanawake wana mikutano yao ambayo inaratibiwa na Kurugenzi. Mikutano hiyo ni pamoja na Halmashauri ya Wanawake, KKKT ambayo inakutana Februari kila mwaka.

Mikutano Mkuu wa Wanawake hufanyika kila baada ya miaka minne. Mikutano ujao unatarajiwu kufanyika mwaka 2014 Julai katika Dayosisi ya Mashariki na Pwani.

Vile vile upo mikutano wa Makatibu Watendaji wa Wanawake wa Jumuiya ya Makanisa ya Kilutheri Kanda ya Katu na Mashariki mwa Afrika (LUCCEA), unaofanyika mara moja kila mwaka.

Upo Mikutano wa Makatibu Watendaji wa Idara za Wanawake wa Makanisa Wanachama wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) unaofanyika mara moja kwa mwaka.

Mikutano wa WCC kufanyika Korea Oktoba

Mikutano Mkuu wa Baraza la Makanisa Duniani (WCC) utafanyika Busan, Korea ya Kusini, Oktoba 2013.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania linatarajiwu kuwakilishwa na: Mkuu wa Kanisa, Askofu Dkt. Alex Malasusa; Bibi Lydia Mbise toka Dayosisi ya Meru; na Bw. Timoth Jonathan Kyelula, toka Dayosisi ya Ulanga - Kilombero.

1963



2013

Askofu Mkumbo asisitiza ushirikiano na uadilifu



Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete katikati ya Mkuu wa KKKT Askofu Dkt. Alex Malasusa na Askofu Dkt. Alex Mkumbo (aliye na fimbo) katika picha ya pamoja na Maaskofu wa KKKT siku Askofu Dkt. Mkumbo alipowekwa wakfu kuongoza KKKT Dayosisi ya Kati.

Askofu Dkt. Alex Mkumbo aliyewekwa wakfu hivi karibuni kuongoza Dayosisi ya Kati ya Kanisa

la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) anaomba ushirikiano toka kwa anaowaongoza ili kutimiza utume wa

Mungu kwa Kanisa wa kueneza Injili.

Katika mahojiano na Gazeti la **Uhuru na Amani**, Dkt. Mkumbo alisitiza ahadi aliyotoa wakati akitikitia wito wa kuongoza Dayosisi ya Kati kwamba atashirikiana na wengine ili kutatua matatizo na changamoto za Dayosisi yake kwa msaada wa Mungu na miongozo ya Kanisa.

Aliwataka wote walio katika nafasi za uongozi kuwa waaminifu, kufanya kazi kwa bidii na kuwa mawakili wema wa mali kidogo inayotokana na michango ya Washarika ili wawaunge mkono na kurejesha imani kwao.

Askofu Mkumbo alisema ingawa kazi ya kuongoza Dayosisi yake ni ngumu lakini kwa kumtii Mungu na maombi toka kwa kila Msharika anaamini mambo yatafanyika inavyotakiwa.

Askofu Dkt. Mkumbo alisimikwa kuwa Askofu wa Dayosisi ya Kati 6 Januari 2013 katika Ibada iliyohudhuriwa na umati mkubwa wa watu katika Kanisa Kuu la Kilutheri Usharika wa Immanuel mjini Singida.

Miongoni mwa walihuduria ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete, Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa; viongozi wa Dayosisi za KKKT; Katibu Mkuu wa KKKT, Bw. Killewa na NKM Misioni na Uinjilisti KKKT, Mch. Ambele Mwaipopo.



uliopo kwa baadhi ya viongozi uondoke nchini.

Sitta alisema Tanzania hivi sasa imegawanyika makundi makundi kutowakana na vitendo vya rushwa na ujisidi kila mahali na hivyo kuwafanya wananchi kukosa imani na baadhi ya viongozi wao.

“Nchi yetu imegawanyika makundi makundi, ukienda bandarini baadhi ya watu wamekalia kuiba tu, katika mabenki hali ipo hivyo na hata vijijini kwenye vyama vya msingi wapo watu wamejawa na unafiki wanataka kuwaibia wakulima,” alisema Sitta.

Alisema hata kwa baadhi ya viongozi kusema uongo wanaona ni jambo la kawaida wakati ni hatari kwa nchi. Haiwezekani mkawa katika uovu na nchi ikawa salama hivyo ni lazima unafiki huo

“Nimekuwa kiongozi ndani ya Serikali za marais wanne kutoka mwaka 1975, nimefanya kazi na hayati Mwalimu Julius Nyerere, Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa na sasa Rais Jakaya Kikwete, haiwezekani mwana siasa, mtoto wa mkulima, ukatajirika ndani ya siasa,” alisema.

Harambee hiyo iliyoonozwa na Mkuu wa KKKT, Askofu Dkt. Alex Malasusa, jumla ya Sh. milioni 132 zilipatikana kati ya Sh. milioni 200 zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa kanisa hilo.

Umuhimu wa kutunza mazingira na uhusiano wake na imani zetu

Na Anicet Maganya

Watu wengi wameongea kuhusu mazingira na utunzaji wake na kufikiri tu kwamba huu ni wajibu wa jamii kufanya kama zinavyofanyika kazi nyingine. Jambo hili si jepesi wala gumi kama watu wengi wanavyofikiri. Ila kwetu **wana-imani** tunavutwa kufikiri nje ya mipaka ya kawaida na kuihusisha **imani yetu**.

Mazingira (maji, miti, wanyama, madini, ndege, samaki, na rasilimali nyingine zote) **ni zawadi toka kwa Mungu**. Mwanadamu na hasa Mkristo kwa lugha ya Biblia **ni wakili wa Mungu** hapa duniani. Na uwakilishi huo hauwezi kuishia tu kwamba **tuliumbwa kwa mfano wake**, bali hata matendo na nia vinatakiwa sana kufanana fanana na Mungu. Mungu alipoumba vitu vyote katika ukamilifu wake na kumkabidhi mwanadamu haikuwa na maana nyingine yoyote zaidi ya kuvitumia, kuvitunza na kuvilinda.

Mpango wa Mungu kuumba ulimwengu na mazingira yake yote haukuwa tu kwa ajili ya faida ya mwanadamu, bali kuufanya ulimwengu upendeze na viumbe vyote viishi kwa kutegemeana. Ila kwa kiwango kikubwa mwanadamu amekuwa mstari wa mbele kuteketeza na kuharibu mazingira/ uumbaji wa Mungu bila kujali kwamba ni kwa hatari kwake pia.

Mkristo au mwanadamu kwa ujumla anatakiwa kufahamu kuwa suala la utunzaji wa mazingira si jambo la vyombo vy ya mamlaka tu bali ni zaidi ya hapo, yaani ni kuufikiria uhusiano wako na Mungu kwa kiwango cha juu sana. Unaposhiriki kuharibu mazingira au

unapokaa kimya wakati ukiona mazingira yanaharibiwa ni dhahiri unaonyesha jinsi usivyomjali Mungu kwa kutotii maagizo yake. **Mkristo anatakiwa kujuliza nini amefanya kuhakikisha mazingira au uumbaji wote wa Mungu unaendelea kama iliviyokusudiwa?**

Mwaka 2011 Kanisa letu liliamua kuwa **kila mwaka** liwe na juma zima la kuhamasisha utunzaji wa mazingira/ uumbaji wa Mungu katika **juma la kwanza mwezi Machi**. Je, Usharika au taasisi ya Kanisa ilifanya nini kuhifadhi au kutunza mazingira siku hiyo? Kwa kuteua **Siku ya Mazingira** si tu kwamba Kanisa linatambua umuhimu wa kushiriki kwa nguvu zote katika utunzaji wa mazingira na uumbaji wote, bali kumkumbusha Mkristo mmoja mmoja kwa nafasi yake kwamba anapaswa na ni wajibu wake wa kwanza kuhakikisha anatunza mazingira. Kwa maneno mengine ni kwamba kama mtu haoni umuhimu wa kutunza mazingira basi anaikana imani yake. Yakobo anatukumbusha juu ya **imani ionekanayo** (Yakobo 2:17), yaani matendo yetu lazima yaonyeshe wazi tuna uhusiano mzuri na Mungu, watu na uumbaji mwengine wote.

Kuna msemo unaosema "**Ukuu wa taifa na maendeleo yake ya kimaadili waweza tambulika kwa jinsi wanyama wake wanavyotendewa**". Maana ya maneno haya si kwa ajili ya kuwalenga wanyama tu, bali kuutazama uhusiano mzima wa mwanadamu na uumbaji wa Mungu. Kama taifa litaonekana halijali sana mambo ya utunzaji wa mazingira na uumbaji kwa ujumla, basi ujue maadili ya taifa hilo na utengamano wa taifa hilo ni wa mashaka.

Jamii inawajibu kulinda na kutunza mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Huu ni wajibu unaozingatia misingi ya imani, kwa kutambua kwamba, binadamu ameumbwa kwa sura na mfano wa Mungu, akajaliwa tunu na fursa mbalimbali za kusaidia kutunza mazingira sanjari na kutoa huduma makini kwa ajili ya watu wa Mungu.

Sasa umefika wakati kwa mfumo wa elimu barani Afrika kuzingatia mila na desturi njema za Kiafrika na maagizo ya imani katika utunzaji mazingira.

Hii ni changamoto kwa waumini wa dini mbalimbali barani Afrika na dunia nzima, kuhakikisha wanatolea **ushuhuda imani yao kwa matendo**, ili kujenga na kudumisha pamoja na kuimarisha misingi ya haki, amani, upendo na mshikamano wa dhati. Na hayo yawe sanjari na kuchuchumilia mchakato wa utamadunisho ili imani isafishe na kuimarisha tamaduni njema za Kiafrika; mintarafu Injili ya Kristo na Kanisa lake.

Kwa kutambua umuhimu wa utunzaji mazingira Kanisa limekuwa likishirikiana na taasisi za kiserikali na zile zisizo za kiserikali katika kutoa elimu na kuona jinsi gani sera na sheria mbali mbali za nchi yetu zinavyoweza kusimamia kikamilifu utunzaji wa mazingira. Jambo kubwa hasa ni kuona kwa pamoja jinsi gani mtu mmoja mmoja, vikundi na jamii wanashirikishwa kwa karibu sana kutunza mazingira, ikiwa ni pamoja na kukabiliana na '**mabadiliko ya tabia nchi**'.

Tunaweza kusema jinsi mtu anavyotunza mazingira ni zaidi ya utii

Endelea uk. 16



Kamati ya Utetezi katika masuala ya Kiuchumi na Huduma za Jamii, KKKT wakiongozwa Askofu Dkt. Stephen Munga (aliyekaa wa tatu kulia) katika picha ya pamoja na Wabunge mjini Dodoma hivi karibuni. [picha na: kitengo cha utetezi, kkkt.]



Mpango wa Mungu kuumba ulimwengu na mazingira yake ni ili kuufanya ulimwengu upendeze na viumbe vyote viishi kwa kutegemeana.

Kamati ya Utetezi yaundwa

Halmashauri Kuu ya KKKT imeunda Kamati ya Utetezi katika masuala ya Kiuchumi na Huduma za Jamii KKKT.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo ni Askofu Dkt. Stephen Munga na wajumbe ni Askofu Isaya Mengele na Mhe. Janet Mmari. Wengine ni Dkt. Adeline Kimambo, Bibi Anna Mghwira na Mchg. Anicet Maganya.

Pia fungua tovuti ya KKKT: www.elct.org kwa maelezo zaidi.

Mazingira

Inatoka uk. 15

wake kwa sheria na mamlaka za hapa duniani, bali inategemea sana mahusiano ya mtu huyo na Mungu. Kama mtu ni mwaminifu kwa Mungu ni wazi atatunza mazingira, maana *katika mazingira tunamwona Mungu wetu alivyo*. Mara nyingi watu waliokata tamaa kiimani na hata kimaisha wamekuwa wakitoa maneno ya kukatisha tamaa pia hata kwa mambo yanayowezekana katika kutunza mazingira.

Mfano ukimwambia mtu ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na uchomaji mkaa unaharibu mazingira, utasikia anakwambia: ‘Sasa tufanyeje? Hatuna umeme wala sola, ni njia ya kuni na mkaa pekee tunaweza kupika.’ Je, ulishajiuliza hata hapo kijijini kwako, ambapo nina hakika wachomaji wa mkaa wote mnawafahamu; ninyi wananchi na Serikali yenu ya Kijiji mlisshawatengea hata eneo la kuotesha miti?

Suala si kuzuia kukata miti, lakini tunapokata tunafanya nini ili kesho tuendelee kuwa na miti? Huu ni mfano tu mdogo wa kuonyesha jinsi tunavyotakiwa kuwa na fikra mbadala za suluhisho bila kukata tamaa bali kutumia vizuri akili na hekima tuliyo zawadiwa na Mungu wetu.

Nawakumbusha Wakristo wote hasa wana-KKKT, hebu tangu sasa amua kuchukua hatua na kuwa mtu wa tofauti katika kutunza mazingira. Mimi na wewe tuamue kuwa mawakili na wafuasi waaminifu wa Mungu kwa kutunza mazingira na uumbaji wote.

Kanisa lahuzunishwa na kifo cha Mchg. Musa

• Aliwahi kuwa Mkuu wa Sinodi ya Kati



Marehemu Mchungaji Thomas Musa aliywahi kuwa Rais wa Sinodi ya Kati ambayo sasa ni Dayosisi ya Kati na Mkuu wa Chuo cha Theologia Makumira 1971 -1975 ambacho sasa ni Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania linahuzuni kutokana na kuitwa mbinguni kwa Mchg. Thomas Musa aliyezikwa Kinampanda Wilayani Iramba, Mkoani Singida, 5 Februari 2013.

Mchg. Musa alikuwa ni Rais Mstaafu wa Sinodi ya Kati 1964 - Juni 1971. Mchg. Thomas Musa alizaliwa Kijijini Mukonkontena Uwanza, Wilayani Iramba Mkoa wa Singida, 6 Desemba 1927 na kubatizwa 12 Agosti 1929 katika Usharika wa Ruruma.

Mwaka 1955 alijuunga na Chuo cha

Kilutheri cha Theologia Makumira ambacho sasa ni Chuo Kikuu cha Tumaini Makumira na alitunukiwa Cheti cha Theologia 1957.

Aliijunga na kuhitimu kozi maalumu ya Diploma ya Theologia iliyotolewa Marangu (Kilimanjaro) 1960 - 1963.

Mchg. Thomas Musa alipata Shahada (BD) na kisha kutunukiwa Shahada ya Uzamifu (Master of Divinity) ya Chuo cha Theolojia cha Augustana, Rock Island, Marekani mwaka 1963.

Kwa maelezo zaidi fungua tovuti ya KKKT: www.elct.org

Ujumbe wa Danmission watembelea KKKT



Ujumbe wa ngazi za juu toka Danmission (Denmark) ukiongozwa na Mwenyekiti wa Danmission, Askofu Peter Fischer-Muller, ulifika Ofisi Kuu ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) iliyopo Arusha tarehe 11 Januari 2013.

Ujumbe huo pamoja na mambo mengine ulibadilishana uzoefu na kutiana moyo na watumishi wa pande zote mbili ili kustawisha utume wa misioni ya Mungu katika mataifa yote.

Picha juu inaonesha menejimenti ya KKKT ikiwa na ujumbe wa Danmission 11 January 2013. Kutoka kushoto Mchg. Rachel Axwesso, Bw. Jens Kaaber Pors, Mchg. Ambele Mwaipopo, Bw. Mallumbo William Mallumbo, Mchg. Mogens Kajaer, Bibi Kristine Kaaber Pors, Askofu Muller, Bibi Rachel Ramadhani na Bw. Mrema (kulia) aliyeongoza majadiliano.

Pia fungua tovuti ya KKKT: www.elct.org kwa maelezo zaidi.

Vitisho na mauaji ya viongozi wa Kanisa

Inatoka uk. 4

d) Kwa mantiki hiyo hapo juu katika kipengele cha a-c, Wakristo wanaitaka Serikali iweke utaratibu wa kugawana machinjio na mabucha kati ya Wakristo na Waislamu ili kila Mtanzania awe huru kujinunulia kitoweo mahali anapotaka.

Sambamba na kuitaka Serikali kufanya hivyo, tunawakumbusha Wakristo wote Tanzania kuelewa kuwa watakuwa hawajavunja sheria yoyote ya nchi wakiamua kujinchinja kitoweo chao wenyewe. Kuhusiana na tangazo hili kwa Wakristo wote, tunaitaka mihihimi ya dola (Serikali na Mahakama) kuheshimu Katiba ya Nchi yetu, na kipekee kuhusiana na jambo hili Ibara ile ya 19.

e) Kwa upande mwengine, kwa kuwa tayari zipo bidhaa za vyakula katika nchi hii ambazo zina nembo ya ‘halal’ na nyingine hazina nembo hiyo, huu ni uthibitisho kuwa vyakula hivyo vimegawanywa kwa kufuata misingi ya imani za kidini. Kwa hiyo, madai ya kugawanya machinjio na mabucha kwa kufuata misingi ya dini sio jambo jipya kwa sasa katika nchi hii.

2.2 Uchomaji wa Makanisa ulioambatanu na vitisho na mauaji ya viongozi wa Kanisa

Kanisa linalaani vikali mauaji ya kidini yanayoendelea kufanya pamoja na vitisho (systematic persecution) kwa viongozi wa Kanisa na Wakristo wote kwa ujumla.

Mtiririko wa matukio mbali mbali ya nyuma yanatudhahirishia kuwa kumekuwepo na mpango wa muda mrefu wa haya yanayotokea sasa hivi. Tarehe 15 Januari 2011, kundi la

Jihadhari na utapeli huu

Na Elizabeth Lobulu

Siku zote tumeaswa na viongozi mbalimbali wa dini tumtegemee Mungu kwa kwa njia ya sala, ibada na toba ya dhati toka moyoni ili kushinda majoribu. Hata hivyo mara nyingi si rahisi kutambua jaribu linalo kunyemelea.

Bwana Yesu *alijaribiwa na Shetani jangwani*, (Marko 1 : 12 - 13); alijaribiwa na wanafunzi wake alipomwambia Petro: “*Rudi nyuma yangu shetani. Huyawazi yaliyo ya Mungu bali ya wanadamu*,” (Marko 8: 33). Pia tunaambiwa Yesu alijaribiwa na *ndugu zake amba walipanga kumkamata wakidhani amerukwa na akili*, (Marko 3: 21).

Shetani hamwogopi mtu au kitu chochote bali anachotaka ni kutumia jaribu kuhakikisha ufalme wake hauvunjwi duniani. Yupo ndugu mmoja akiongea kuhusu majoribu aliwahi kusema kwamba amejifunza kwa

Waumini wa Kiislamu walipokutana katika ukumbi wa Diamond Jubilee, miongoni mwa walikuwamo mashehe, walijadili hali ya nchi ya Tanzania kuongozwa kwa mfumo wa kidini. Mkutano huo ulihitimishwa kwa kutoa tamko dhidi ya kile kilichoitwa mfumo Kristo katika nchi yetu!

Japo Serikali na vyombo vyake vya usalama wa Taifa vimekuwa vikipata taarifa za vitisho dhidi ya viongozi wa Kanisa, mauaji, kuchomwa kwa nyumba za ibada, pamoja na maneno ya uchochezi kupitia miadhara, vipeperushi, CD na vyombo vya habari vinavyomilikiwa na taasisi zinazofahamika, hata hivyo Serikali kwa kiasi kikubwa imeshindwa kuchukua hatua kwa wakati muafaka na wanasubiri hadi maovu yatendeke ndipo ati waanze kufanya uchunguzi.

Kwa Serikali yetu inaonekana wazi kuwa katika hili ile methali kwamba: “Kinga ni bora kuliko tiba” haina maana yoyote. Hii ni kuonyesha udhaifu mkubwa wa vyombo vya usalama wa Taifa au pia kwamba vyombo hivi vinafurahia kutoweka kwa amani nchini mwetu, jambo ambalo linalifanya Kanisa nchini Tanzania liamini kwamba matukio haya yanayoendelea kutokea ni dalili kuwa Serikali ina agenda ya siri dhidi ya Ukristo. Kutokana na hayo Jukwaa la Wakristo Tanzania linatamka kama ifuatavyo:

a) Tunatambua kwamba ni jukumu la Serikali kuwatendea raia wake kwa usawa na bila ya ubagizi kwa mujibu wa Ibara ya 12 na 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Viongozi wa Kanisa wanamatamka kwamba Serikali imeshindwa kuheshimu Katiba juu ya hizi haki za raia wake na kupelekea waamini

gharama kubwa kushinda majoribu yanayoletwa kwa njia ya utapeli. Yeye sasa anasema: “Hata akiona jaribu linavuka barabara analitambua.”

Wapo matapeli wa kimataifa toka Nigeria amba wanatumia mbinu mbalimbali kuiba fedha za watu.

Barua pepe ya mtu unayemfahamu

Mbinu ya kwanza ni ile ya kutuma barua pepe inayosema, kwa mfano: ‘Mchungaji anayeitwa jina fulani ni mgonjwa au mke wa Askofu fulani amelazwa hospitali na anahitaji dola za Marekani 2,000 atoke hospitali. Kwa hiyo kwa vile unamfahamu unaombwa uchangie sh. 80,000.’ Kwa walio na fedha kama hizo wanaweza kujaribiwa kutuma fedha na zikapotea.

Itaendelea toleo ijalo.

wa dini ya Kikristo kukosa imani na Serikali iliyoko madarakani, hasa kuhusu ulinzi na usalama wao na mali zao kama inavyoagizwa kwenye Ibara ya 14 ya Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. b) Kwa kuwa ulinzi wa raia ni haki ya kikatiba na kisheria, Serikali inatakiwa iwalinde raia wake. Kama Serikali imeshindwa kuwalinda raia wake, Kanisa linataka Serikali ikiri hivyo ili Kanisa liwaambie wananchi waiwajibishe Serikali na Viongozi wanaofanya Serikali ishindwe kutimiza wajibu wake. Jukwaa la Wakristo linasema: Kama Serikali haitachukua hatua za makusudi dhidi ya mambo haya yaliyoainishwa hapo juu, Kanisa litachukua hatua ya kuwaambia waamini wake kwamba Serikali iliyoko madarakani inaibea dini moja, na hivyo Kanisa litatafakari upya uhusiano wake na Serikali.

3. Wakristo walioko Zanzibar

Wakristo walioko Zanzibar wanatishiwa maisha yao na mali zao zinaharibiwa mara kwa mara, kiasi cha wengine kuamua kuhamia Tanzania Bara. Kigezo cha unyanyasaji huo ni suala la udini na muungano. Inaonekana ni kama vile Watanzania waliozaliwa Bara hawana haki ya kuishi Visiwani. Na kumbe wale waliozaliwa Visiwani wafikapo Barani wana haki zote. Kanisa linaitaka Serikali iwhakikishie Wakristo walioko Zanzibar usalama wao na wa mali zao maana hiyo ni haki yao ya Kikatiba.

4. Vitisho na mauaji ya Wanakanisa

Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania ichukue hatua za makusudi za kuzuia vitisho na mauaji kwa Viongozi wa Kanisa na Wakristo kwa ujumla. Vinginevyo Kanisa litautangazia ulimwengu kuwa Tanzania ni nchi mojawapo inayovunja haki za binadamu kwa ubagizi wa kidini na kulitesa Kanisa kimfumo.

5. Matumizi ya Vyombo vya Habari:

Kwa kuwa kuna baadhi ya vyombo vya habari ambavyo vimeruhusu vitumiwe kuwatukana Viongozi wa Kanisa, tunatoa nafasi kwa vyombo hivyo kuomba radhi; vinginevyo tutaitaka dunia ivielewe kuwa navyo ni sehemu ya chanzo cha migogoro. Pia tunachukua nafasi hii kuvitahadharisha vyombo mbalimbali vya habari kupima kwa kina ni nini kinachosemwa na viongozi wa kidini ili kuviepusha vyombo hivyo kutumika kwa nia ya uchochezi, yasije yakutukuta kama yale yaliyotokea kule Rwanda 1994.

6. Hitimisho:

Kanisa linaendelea kusisitiza kuwa silaha kuu ya Mkristo katika nyakati hizi ni maombi na kufunga. Kwa mantiki hiyo, Kanisa linawataka Wakristo wote nchini Tanzania kuungana kwa pamoja katika maombi na kufunga kwa kwa ajili ya hali hii ilijojitokeza hapa nchini.

Soma kwa kirefu toleo katika tovuti ya CCT:
<http://cct-tz.org/>

SOMO LA BIBLIA

Kutubu na kurejea kwa Bwana

Zab 51: 1- 10

Na Mchg. Rachel Axwesso

Kila mwaka tumekuwa na siku inayoitwa ya "Jumatano ya Majivu". Je ina maana gani? Ni siku muhimu kwa kila Mkristo. Ni wakati wa kutafakari na kukagua maisha yetu. Pia ni kipindi cha kuchunguza kwamba ni wapi niko/ niko nje ya mstari katika ukristo wangu. Wapi nimetenda isivyo sawa na kumhuzunisha Mungu kwa matendo yangu. Hivyo ni kipindi muhimu sana.

Zaburi ya 51 ni mojawapo ya sala ya Mfalme Daudi kwa Mungu. Daudi ni Mfalme wa pili kutawala Taifa la Israeli. **Daudi alitembea na Mungu katika maisha na alifanikiwa sana.** Kwa kweli **alipata kibali machoni pa Mungu na kuwa muhimili katika Taifa la Mungu.** **Shetani naye alikuwa anatembea na Daudi.** Na ndivyo alivyofanya kwa Ayubu, mtu aliyekuwa mcha Mungu, mwelekevu na mwadilifu.

Shetani alipopata nafasi aliingia na kumwangusha Daudi; (*pepo la uzinzi, uasherati, umwagaji damu likamshika Daudi*). Kwa sababu hiyo Daudi alimwacha Mungu na kumwasi - Mungu aliye asili ya mafanikio yake.

Shetani haogopi mafanikio yako, hekima, cheo, mali, umri, nk. Shetani anamwogopa mtu anayesali, anayeomba kwa kumaanisha, na anayesoma na kuliamini Neno la Mungu. Martin Luther aliamini na kusema: "Afadhalii kupigana na askari 1,000 wenye silaha kuliko upigane na Mkristo mmoja anayeomba Mungu." Mtu mwenye Neno na sala ni hatari kwa shetani na Shetani anamwogopa sana.

Matokeo ya kumwacha Mungu

Dhamira inadhoofika, au kufa kabisa. Utamjua kwa kutazama matendo yake; Hofu ya Mungu inamtoka; na Roho Mtakatifu anamwacha kwa sababu ya maovu yanayo mhuzunisha; Pia milango ya kutoa au kupokea msamaha inajifunga na juhudhi ya kutafuta uso wa Mungu kwa toba inakwisha.

Biblia inatuambia, "**Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya, basi nitasikia toka mbinguni na kuwasamehe dhambi yao na kuionya nchi yao.**" (2Nyakati 7: 14). Mfalme Daudi alikengeuka, moyo wake ulishikwa na tamaa mbaya, alifanya uasherati na hatimaye alimwaga damu ya Uria, mtu asiyé na hatia yoyote. Kumbuka kwamba kweli dhambi ni

mzigo mzito. Daudi alilemewa na dhambi. Unajua dhambi ina tabia ya kuita dhambi nyingine usipotubu. (Inafananishwa na ndizi kinango – haizai hadi itakapokuwa na mashina mengi). Hili ndio lililomtokea Daudi. Jeshi lake chini ya Kamanda Yoabu lilikuwa vitani na Uria mmoja wapo wa wapiganaji. Daudi akavamiwa na tamaa ya kumchukua mke wa Uria (Bethsheba mzuri wa sura) kwa kutumia cheo chake.

Matunda ya dhambi yalipozaliwa, akaanza mazingira ya kuficha uovu kwa mwanadamu (siyo kwa Mungu aonaye hata yanayotendwa gizani). Kwa maana imeandikwa, "**Mungu ataleta hukumuni kila kazi na kila neno la siri,**" (Mhu 12: 13 -14). Daudi alijaribu kila mbinu kuficha dhambi zake. Alitura ujumbe kwa Yoabu Kamanda wa Jeshi ampe Uria ruhusa ya kusalimia familia yake. Uria aligoma siku zote mbili – akalala na walini wa mfalme.

Mbinu zote ziliposhindikana Daudi aliandika barua na kuituma kwa Yoabu – kwa mkono wa Uria ikimweleza: "**Mwekeni Uria mbele ya watu penye vita kali kisha ondokeni, mwacheni, apigwe afe.**" (2Sam 11:15b). Yoabu alitekeleza agizo la mkuu – Uria akapoteza uhai kwa hila.

Wakati wote jicho la Mungu lilimtazama Daudi. Mungu aliruhusu kifo cha Uria ili aweze kupidisha neema na rehema zake kwa Daudi. Mtumishi wake (aliyekubali kutubu na kurejea kwa Mungu). Mungu ametengeneza milango ya toba na baraka kwa namna ya ajabu sana. Hakika dhambi inanuka sana. Ina piga kelele. Biblia inatuambia, "lakini jambo lile lilimchukiza Mungu (Bwana)," (2Sam 11: 27c). Ujumbe wa Mungu – Nathan (2Sam 12: 1- 9). Hakika mshahara wa dhambi ni mauti (Rum 6: 23).

Toba ni dawa ya dhambi

Kipimo utakachopima kwa mwenzako ndicho utakachopimiwa. Apandacho mtu ndicho atakachokivuna. Neno la Mungu kwa Daudi: "**Nitatwaa wake zako mbele ya macho yako na kumpa jirani naye atalala na wake zako mbele ya jua hili,**" (2Sam 12: 11). Kumbuka katika mzunguko wote, Daudi alikutana na neema ya Mungu, akatambua dhambi zake. Ujue si kwa njia rahisi bali kwa gharama kubwa.

Epuka kujaribu dhambi

Tunahitaji kusikiliza vizuri - tusikie Neno na maonyo ya Mungu. Kumbuka ukweli

kwamba *chakula cha uovu ni kitamu lakini mdomo huja changarawe. Utamu unapotea na kusahaulika, uchungu unabaki.* Ona uchungu uliotokea kwa Mfalme. Mtoto wa Daudi wa uezee aliukufa. Amnoni alimbaka Tamari. Absalmon alipanga na walini na kumuua Amnoni. Absalmon aliuawa kwa kutupwa shimonii na kuuliwa na chungu lenye mawe mazito.

Maisha ya Daudi baada ya uovu

Hakuwa na usalama. Hayakuwa mazuri kwa sababu maadui waliinuka. Mikosi, vifo, huzuni, maombolezo, bila fahari. Akapata mfadhaiko kwa sababu ya dhambi. Utawala ukayumba. Kumbuka dhambi ina madhara makubwa sana. Dhambi inaharibu na kuangamiza kabisa.

Toba ni bora

Daudi alimwambia Mungu "**nimekosa kwa haya niliyotenda, nimefanya upumbavu, niondolee uovu.**" Akavunjika, akaweka moyo wake wazi kwa Mungu: *Nimekukosa, nimepotoka na mkono wako u juu yangu,*" (2 Sam 24:17). **Nimetenda dhambi juu ya macho yako** (Zab 51: 4). Daudi aliomba toba na rehema kwa Mungu "**Kiasi cha wingi wa rehema zako, uyafute makosa yangu,**" (Zab 51: 1). Ndugu yangu katika suala la toba usimwangalie mwanadamu, utakata tamaa bali umtzame Mungu. Daudi angeangalia watu, yeche kama mkuu, kiongozi wa nchi, asingelitubu maana angeona marafiki, watoto, wake zake, nk., asingelitubu.

Iko faida ya kusamehewa dhambi

Unakuwa mtu huru. Mtu mpya. Chombo cha kuwatia moyo watu wakosaji *waliolemewa na mizigo ya dhambi.* Msamaha unaongeza uhai. Daudi alitubu kwa machozi. Mungu akamsamehe.

Msamaha ni afya

Daudi akaona mwisho mwema, akashiba miaka (2Fal 1:1). Wapendwa "**tubuni, basi, mrejee ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuja kwake Bwana,**" (Mdo 3: 19). Nenda Kalvari na mzigo wako wa dhambi, uutue, usijiliwaze na dhambi, ukidhani uko salama, ni hatari.

Kagua maisha yako, tengeneza mahusiano yako na Mungu na wanadamu pia. Yeye atakurehemu. Mungu akubariki. Amen.

Ifahamu

Radio Sauti ya Injili

Inasikika:

Morogoro 99.6 MHz

Mlalo, Lushoto 102.6 MHz

Moshi 97.2 MHz Arusha 96.2 MHz

Same 100.4 MHz Kibaya 102 MHz

Kidia, Old Moshi 92.2 MHz

Hakwe, Rombo 96.4 MHz

Masafa Mafupi SW asubuhi na usiku tu:

MHz 7275 na MHz 9475

Satellite:

C- Band Intelsat 602 63 Degrees East - chini ya MNet Channel
KU Band-Pas 10 digital 68.5 Degrees East

Mawasiliano:

Mkurugenzi RSYI

S.L.P. 777

Moshi, Tanzania

Barua Pepe: redio@elct.org

Simu: +255 275 27 72

+255 272 753 080

Sikiliza kupitia tovuti:

Tovuti: www.redio@elct.org

HABARI PICHA



Hivi karibuni watu walijitokeza kwa wingi katika harambee kuanza kuchangia fedha za kukarabati jengo la Kanisa la KKKT Usharika wa Mbagala, Temeke jijini Dar es Salaam lili洛homwa moto na wafiasi wa Kiislamu. Ukarabati utaenda sambamba na ujenzi wa Kituo cha Amani na kuweka uzio ambapo kwa pamoja vitagharimu sh. bilioni 6 hadi kukamilika. (Juu Kushoto) Mkuu wa KKKT ambaye pia ni Mkuu wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Askofu Dkt. Alex Malasusa.

(Kulia) washarika wa Mbagala waliohuzunishwa na kitendo cha kanisa lao kuharibiwa.

Baada ya Bw. Uhuru
Kenyatta (Kulia)
kutangazwa na Tume
Huru ya Uchaguzi
na Mipaka kwamba
ameshinda kiti cha Urais
nchini Kenya, kuna
dalili kwamba upigaji
kura utarudiwa kati yake
na Bw. Raila Odinga
ambaye amepeleka kesi
mahakamani kupinga
matokeo.



Papa Francis wa I
(Kushoto) ambaye
alisimikwa 20 Machi
kuongoza Kanisa
Katoliki duniani,
awataka viongozi
wasipende anasa
bali wajali zaidi
kuwasaidia watu
maskini.



Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya KKKT waliokutana hivi karibuni ili pamoja na mambo
mengine, kuona jinisi ya kutunza mvutano katika Dayosisi ya Kaskazini Kat.